BU African Studies Center LANGUAGE PROGRAM, 232 BAY STATE ROAD, BOSTON, MA 02215 africa@bu.edu
www.bu.edu/Africa/alp 617.353.3673

**Asiyesikia La Mkuu …**

| | |
|---|---|
| **Mama Rukia:** | Karibuni chai wanangu, kunyweni haraka haraka ili muwahi shule. |
| **Rukia & Ali:** | Asante mama. |
| **Mama Rukia:** | Karibu chai baba, |
| **Baba Rukia:** | Asante mama. |
| **Rukia & Ali:** | Mama, chai ya leo ni ya moto! |
| **Mama Rukia:** | Na nyie mnadeka sana kunyweni chai haraka haraka ili muwahi shule. |
| **Baba Rukia:** | Haya pulizeni basi hiyo chai. Wanangu jaribuni kumaliza chai mapema ili muwahi shule. Rukia unajua huu ndiyo muhula wako wa mwisho…, |
| **Rukia:** | Ndiyo baba. |
| **Baba Rukia**: | Mnakwenda kufanya mitihani…, |
| **Rukia & Ali:** | Ndiyo baba. |
| **Baba Rukia:** | Mimi nategemea mitihani ya mwaka huu mtafanya vizuri na (Rukia)utakwenda chuo kikuu na hapo baadaye Mungu akipenda utakuwa daktari. Jitahidi sana kusoma si unapenda kuwa daktari? |
| **Rukia:** | Ndiyo baba napenda. |
| **Baba Rukia:** | Elimu ni kila kitu hapa duniani. |
| **Rukia:** | Asante baba. |
| **Baba Rukia:** | Na wewe bwana mdogo unasoma? |
| **Ali:** | Ndiyo baba nasoma! |
| **Baba Rukia:** | Kweli unasoma? muhula uliopita ulipata ngapi? Alama gani? |
| **Ali:** | Kweli baba nasoma, muhula uliopita nilipata alama B. |
| **Baba Rukia:** | Vizuri sana jitahidi sana, muhula ujao nataka upate A. |

© Boston University

**Baba Rukia:** Haya, chukueni hii hela ya nauli mpande basi siyo vizuri kuomba lifti.

**Rukia & Ali:** Sawa baba.

**Baba Rukia:** Haya msome salama.

**Rukia & Ali:** sawa baba, asante.

**Baba Rukia:** Naona vijana wamejiandaa vizuri.

**Mama Rukia:** Ndiyo kabisa, wamejiandaa vizuri.

**Baba Rukia:** Wanapenda kusoma sana, nafikiri mara kwa mara tushauriane ili tuweze kuwasaidia hawa vijana wetu.

**Mama Rukia:** Sawa kabisa baba.

**Baba Rukia:** Mama Rukia, ngoja mimi niende kazini.

**Mama Rukia:** Sawa baba.

**Baba Rukia:** Mchana mwema.

**Mama Rukia:** Asante na wewe pia

***Baada ya siku mbili***

**Mama Rukia**: Baba Rukia, karibu maji maana kuna joto kweli.

**Baba Rukia:** Asante sana mama Rukia.

**Mama Rukia:** Habari za kazi ? Na unaendeleaje kazini?

**Baba Rukia:** Kazi zimeenda vizuri tuu, tulikuwa tuna kazi nyingi, lakini pia tumeweza kusafirisha ule mzigo.

**Mama Rukia:** Hongera sana.

**Ali:** Hodi hapa?

**Baba na mama:** Karibu

**Baba Rukia:** Habari za shule?

**Ali:** Nzuri tuu

**Baba Rukia:** Vipi mwenzako yuko wapi?

**Ali:** Nilimwacha na marafiki zake shuleni wanasoma,nikamwambia twende nyumbani, akaniambia kwamba anasoma.

**Mama Rukia:** Umesema ameenda kusoma na wenzake?

**Ali:** Ndiyo mama.

**Mama Rukia:** Haya nenda kuna chakula jikoni ukale.

**Baba Rukia:** Umesema marafiki zake gani?

**Ali:** Alikuwa na marafiki zake wakielekea gengeni.

**Baba Rukia:** Hii ni hadithi au maneno?

**Mama Rukia:** Haya ni maneno tuu kwasababu hii siyo mara ya kwanza Rukia kuchelewa nyumbani hata kipindi kile ulivyosafiri alikuwa anachelewa kurudi.

**Baba Rukia:** kwahiyo unasema ni kujisomea, lakini hukuniambia kama anachelewa kila siku.

**Mama Rukia:** Siyo kama anachelewa kila siku, siku nyingine anawahi kurudi.

**Baba Rukia:** Mama Rukia zungumza na binti yako! Umenielewa?

**Mama Rukia:** Ndiyo baba, siku nyingine akichelewa kurudi ananiambia anajisomea na wenzake

***Baada ya dakika chache***

**Mama Rukia:** Kwanini unaingia nyumbani kwenu kwa kunyatanyata?
Hebu njoo hapa, inathibitisha ulikuwa unanyatanyata, na viatu umeshika mkononi

**Baba Rukia:** Viatu vimekatika?

**Rukia:** Hapana baba.

**Mama Rukia:** Ulikuwa wapi mpaka sasa hizi?

**Rukia:** Nilikuwa kwenye masomo ya ziada na rafiki zangu

| | |
|---|---|
| **Baba Rukia:** | Rukia saa hivi ni saa ngapi? Inakaribia saa mbili za usiku mtoto wa kike! |
| **Rukia:** | Baba nilikuwa najisomea na marafiki zangu, nilikuwa nikisubiri mwalimu utakeyenitafutia. |
| **Baba Rukia:** | Una uhakika? |
| **Rukia:** | Ndiyo baba, najisomea. |
| **Baba Rukia:** | Kwenye mgahawa? |
| **Rukia:** | Hapana baba tulikuwa tunajisomea pale tukasika kiu. |
| **Mama Rukia:** | Mbona ndugu yako anasema ulikuwa na vijana ambao hawafahamu? Rukia mwanangu! |
| **Rukia:** | Siyo vijana peke yake tulikuwa mchangayiko. |
| **Mama Rukia:** | Rukia mwanangu hii tabia unayoianza siyo nzuri kumbuka hii siyo mara yako ya kwanza kurudi nyumbani usiku. Kumbuka unatakiwa usome, elimu ndiyo urithi wako wa baadaye, habari kwenye mgahawa achana nazo mwanangu. |
| **Mama Rukia:** | Kuna magonjwa mengi sana kama vile ukimwi kwahiyo achana nayo. Sawa mama? |
| **Rukia:** | Nisamehe wazazi wangu sitarudia tena kuja saa kama hizi, nitawahi kidogo. |
| **Baba Rukia:** | Saa hizi umekujaje mtoto wa kike na umepataje daladala |
| **Rukia:** | Rafiki zangu wana magari. |
| **Mama Rukia:** | Si, nilikukataza kupanda magari tofauti na daladala? Magari ya ovyo ovyo na unapanda magari ya mtu ni mtu tuu. |
| **Mama Rukia:** | Ile hela baba aliyonipa niliibiwa kwenye daladala kwa hiyo niliomba lifti, kwa hiyo tulivyomaliza masomo ya ziada na wenzangu nilisubiri wanipe lifti, na miguu ikawa imechoka ndiyo maana nikavua viatu. |
| **Mama Rukia:** | Nenda jikoni ukale. |

***Siku ya tatu***

**Ali:** Hodi mama?

**Mama Rukia:** Karibu.

**Ali:** Shikamoo mama.

**Mama Rukia:** Marahaba, habari za shule?

**Ali:** Nzuri tuu mama, kuna barua nimepewa kutoka shuleni na mwalimu mkuu.

**Mama Rukia:** Inahusu nini?

**Ali:** Sijaweza kufungua mama.

**Baba Rukia:** Hodi hapa.

**Mama Rukia:** Karibu.

**Ali:** Shikamoo baba,

**Baba Rukia**: Marahaba mwanangu, mbona bahasha kubwa?

**Ali:** Nimepewa na mwalimu  mkuu, nikaambiwa nifikishie wazazi.

**Baba Rukia:** Mwalimu mkuu? Umeisoma?

**Mama Rukia:** Hapana, ndiyo kwanza nimeipokea sasa hivi.

**Baba Rukia:** Hebu tuisome, hebu soma kwa nguvu.

**Mama Rukia**: Mungu wangu!

**Baba Rukia:** Wewe mama Rukia! Nini?

**Mama Rukia:** Rukiaa…

**Rukia:** Bee mama.

**Baba Rukia:** Nini?

**Rukia:** Shikamoo baba, shikamoo mama.

**Baba & Mama Rukia**: Marahaba

**Mama Rukia:** Rukia mwanangu ndiyo umefanya nini sasa?

**Rukia:** Mama, najuta mama.

**Baba Rukia:** Unajuta nini?

**Rukia:** Naomba mnisamehe…

**Baba Rukia:** Nimelipa pesa nyingi kwa ajili yako.

**Rukia:** Naomba nisamehe baba…

**Baba Rukia:** Miaka yote umesoma zimebaki siku tatu ufanye mtihani!

**Rukia:** Baba naomba unisamehe…

**Baba Rukia:** Kweli umeenda kufanya mchezo kama huo?

**Rukia:** Baba nisamehe, sikutegemea…

**Baba Rukia:** Nitaweka wapi uso wangu mimi katika dunia ya leo?

**Rukia:** Baba yangu naomba nisamehe…

**Mama Rukia:** Nimekukataza magenge mwanangu.

**Rukia:** Mama naomba nisamehe...

**Baba Rukia:** Hukusikia nilichokuambia mwanangu? Leo unaamini hilo.

**Rukia:** Nisamehe baba yangu sitarudia tena.

**Baba Rukia:** Nilikuambia asiyesikia la mkuu huvunjika guu na leo umeyaona?

**Rukia:** Wazazi wangu naomba mnisamehe nipo chini ya miguu yenu.

**Mama Rukia:** Aibu gani hii mwanangu?